





Uamuzi

La décision

-  Ursula Nafula
-  Vusi Malindi
-  Ursula Nafula
-  Kiswahili / French
-  Level 2

(imageless edition)






Kijiji changu kilikuwa na matatizo mengi. Tulipanga foleni ndefu tukisubiri kuchota maji kutoka mfereji mmoja.

...


Mon village avait plusieurs problèmes. Nous faisons la file pour aller chercher de l'eau d'un seul robinet.



Tulisubiri kupokea msaada wa
chakula.

...


Nous attendions la nourriture
donnée par les autres.



Tulifunga nyumba zetu mapema
kwasababu ya wizi.

...


Nous avons barré nos maisons tôt
à cause des voleurs.



Watoto wengi waliacha shule.

...


Plusieurs enfants avaient lâché
l'école.



Wasichana wadogo walifanya kazi
kama watumishi kwenye vijiji
vingine.

...


Les jeunes filles travaillaient
comme domestiques dans d'autres
villages.



Wavulana wadogo waliranda randa
kijijini na wengine walifanya kazi
kwenye mashamba ya watu.

...


Les jeunes garçons se promenaient
autour du village pendant que
d'autres travaillaient sur des
fermes.



Upepo ulipovuma, ulipeperusha
karatasi chafu na kuzifikisha mitini
na uani.

...


Quand le vent soufflait, des
déchets de papier pendaient des
arbres et des clôtures.



Watu walikatwa na vipande vya
chupa vilivyotupwa ovyo ovyo.

...


Les gens se faisaient couper par de
la vitre brisée lancée sans faire
attention.



Halafu siku moja, mfereji wa maji ulikauka na mitungi yetu ikawa kawa tupu.

...


Puis un jour, le robinet se tarit et nos conteneurs étaient vides.



Baba yangu alitembea kutoka
nyumba hadi nyumba akiwaomba
watu kuhudhuria mkutano wa kijiji.

...


Mon père marcha de maison en
maison et demanda aux gens de
participer à une réunion du village.



Watu walikusanyika chini ya mti
mkubwa na kusikiliza.

...


Les gens se recueillirent sous un
grand arbre et écoutèrent.



Baba yangu alisimama na kusema,
“Tunahitaji kusaidiana kutatua
matatizo yetu.”

...


Mon père se leva et dit, « Nous
devons travailler ensemble pour
résoudre nos problèmes. »



Juma, mtoto wa miaka minane aliyekuwa amekaa kwenye tawi la mti, alisema kwa sauti, “Naweza kusaidia na usafi.”

...


Juma, âgée de huit ans et assise sur un tronc d’arbre, cria, « Je peux aider à nettoyer. »



Mwanamke mmoja alisema, “Sisi wanawake tunaweza kuungana na kuotesha chakula.”

...


Une femme dit, « Les femmes peuvent me joindre pour cultiver de la nourriture. »



Mwanamume mwingine alisimama
na kusema, “Wanaume
watachimba kisima cha maji.”

...

Un autre homme se leva et dit, «
Les hommes creuseront un puits. »



Sote tulisema kwa sauti moja,
“Lazima tubadilishe maisha yetu.”
Tangu siku hiyo, tulifanya kazi
pamoja kutatua shida zetu.

...

Nous criions tous avec une voix, «
Nous devons changer nos vies. »
Depuis ce jour, nous avons travaillé
ensemble pour résoudre nos
problèmes.



Storybooks Canada

storybookscanada.ca

Uamuzi

La décision

Written by: Ursula Nafula

Illustrated by: Vusi Malindi

Translated by: (sw) Ursula Nafula, (fr) Alexandra Danahy

This story originates from the African Storybook (africanstorybook.org) and is brought to you by Storybooks Canada in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 4.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/).